HALIUZWI

# Jarida la NEMC


BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

ISBN 0856 - 6933 | TOLEO NA. 009 | OKTOBA - DISEMBA, 2022


## TANZANIA YASHIRIKI MKUTANO WA UMOJA WA MATAIFA WA MABADILIKO YA TABIANCHI



Ndani:

- MAKAMU WA RAIS AFUNGUA MKUTANO WA UMOJA WA MATAIFA JUU YA TATHMINI YA HALI YA MAZINGIRA YA BAHARI
- OPERESHENI YA KAMATA MIFUKO YA PLASTIKI ISIYO RASMI YAZINDULIWA - NA MKUU WA MKOA DAR ES SALAAM, MAKALA
- MAKALA: BANDARI ZISIZOKUWA RASMI NA CHANGAMOTO KWENYE MAZINGIRA

@nemctanzania

NemcTVTanzania

www.nemc.or.tz

#MazingiraYetuUhaiWetu

# YALIYOMO


003 NEMC YASHIRIKI MAONESHO YA UWEKEZAJI NA UZINDUZI WA VIWANDA NA BIASHARA - PWANI

004 WAZIRI JAFO ASHIRIKI KAMPENI YA USAFI WA FUKWE ZA RAINBOW MKOANI DAR ES SALAAM

005 NEMC YATEKELEZA AGENDA YA KIMATAIFA YA “MAENDELEO ENDELEVU YA MILIMA”

006 JAFO AHIMIZA UTUNZAJI NA UHIFADHI WA MAZINGIRA- KISARAWE

008 WAZIRI JAFO ATOA SIKU TANO KWA KIKOSI CHA KUSIMAMIA MUONGOZO WA USAFISHAJI WA MCHANGA CHA MKOA WA DAR ES SALAAM

009 GEREJI BUBU KERO KWA WANACHI NA CHANZO KIKUBWA CHA UCHAFUZI WA MAZINGIRA NCHINI

010 ATHARI ZA UCHIMBAJI MADINI KWENYE MAZINGIRA





11 Tanzania yashiriki Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi

012 NAFASI YA MAENEO YA BINADAMU NA HIFADHI HAI KATIKA KUHIFADHI MAZINGIRA

013 WAZIRI JAFO ASHIRIKI ZOEZI LA KUPANDA MITI KATIKA WILAYA YA BAGAMOYO

015 MAGARI YA TAKA NI CHANZO CHA UCHAFUZI WA MAZINGIRA

016 UTUNZAJI NA UHIFADHI WA MAZINGIRA KATIKA UCHIMBAJI WA MADINI

017 IFAHAMU KWA UNDANI TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA(TAM)

020 Kauli ya Mazingira

022 Kauli ya Mazingira: Katuni


## UTANGULIZI

### BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilianzishwa kwa Sheria ya Taifa ya Usimamizi wa Mazingira Na. 19 ya mwaka 1983 kama chombo cha kuishauri serikali juu ya masuala ya utunzaji endelevu wa Mazingira. Baraza lilianza kazi rasmi mwaka 1986. Sheria Na. 19 ya mwaka 1983 ilifutwa mwaka 2004 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 (Sura 191) ambayo ilianzisha Baraza kwa mara nyingine.

Tangu kuanzishwa kwake, Baraza limekuwa likisimamia na kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu suala zima la hifadhi ya mazingira na maendeleo endelevu nchini. Kwa mujibu wa kifungu cha 17 cha Sheria hiyo, madhumuni na sababu za kuanzisha Baraza hili ni kuratibu utekelezaji wa Sera na Sheria ya Mazingira katika nyanja kuu nne ikiwa ni pamoja na:-

1. Kutekeleza shughuli za uzingatiaji na utekelezaji (enforcement and compliance) wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;
2. Kusimamia mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) (Kuratibu, kufanya mapitio ya ripoti za TAM kutoka kwa wenye miradi na kufuatilia utekelezaji wake);
3. Kufanya tafiti za mazingira; na
4. Kuwezesha ushiriki wa umma katika kufanya uamuzi unaohusu mazingira na kusimamia kwa ujumla na kuratibu masuala yote yanayohusu Mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Sheria nyingine zozote zilizoandikwa.


**BODI YA UHARIRI:**

**Mwenyekiti:**
Dkt. Menan Jangu

**Mhariri Mkuu:**
Irene John

**Wachangiaji:**
Monica Sapanjo
Dalia Charles
Rose Mtui
Martha Kawishe
Pendo Kundya
Neema Mdimi
Hilda F. Mwakasungura

**Msanifu Michoro:**
Blasius Haule

# NEMC YASHIRIKI MAONESHO YA UWEKEZAJI NA UZINDUZI WA VIWANDA NA BIASHARA - PWANI



Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limeshiriki maonesho ya wiki ya uwekezaji na uzinduzi wa viwanda na biashara yaliyofanyika katika viwanja vya Mailimoja Mkoa wa Pwani Kibaha kwa kutoa elimu ya Mazingira kwa kuzingatia Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake katika sekta ya viwanda na Biashara.

Maonesho hayo yaliyozinduliwa na Rais Mstaafu wa awamu ya nne Mhe Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete yamelenga katika Mkoa wa Pwani kuwekeza katika viwanda ili vijana waweze kujiajiri na Tanzania iweze kukua kwa uchumi endelevu.

Akizungumza katika uzinduzi huo Mhe Dkt Jakaya Kikwete alisema azma ya Serikali ya awamu ya Sita ya Mhe.Samia Suluhu Hassan ni dhahiri na yenye lengo chanya la kukuza uchumi endelevu kwa kuwekeza katika viwanda na Biashara hali itakayowawezesha vijana wa Kitanzania kujihusisha na ujasiriamali ili waweze kujikwamua katika maendeleo.



Naye Mhandisi Mwandamizi NEMC Bi.Luhuvilo Mwamila kwa niaba ya Meneja NEMC Kanda ya Mashariki Kaskazini alipozungumza alisema lengo la ushiriki wa NEMC katika maonesho haya ni kutoa elimu kwa wamiliki wa viwanda na watanzania kwa ujumla juu ya utunzaji na uhifadhi wa Mazingira katika sekta ya viwanda kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake.

Haya ni maonesho ya tatu ya viwanda na Biashara kufanyika katika Mkoa wa Pwani yanayoenda sambamba na kaulimbiu isemayo

***"Pwani ni sehemu sahihi kwa uwekezaji, pamoja tujenge viwanda kwa uchumi na ajira endelevu"***

# WAZIRI JAFO ASHIRIKI KAMPENI YA USAFI WA FUKWE ZA RAINBOW MKOANI DAR ES SALAAM



*Waziri wa Nchi Muungano na Mazingira Mhe. Dkt Selemani Jafo ......*

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt Selemani Jafo alishiriki katika kampeni ya usafi wa fukwe za Rainbow zilizopo katika Manispaa ya Kinondoni katika Mkoa wa Dar es Salaam. Kampeni hiyo inaitwa ***zero plastic*** ikiwa ni juhudi za kutokomeza kabisa matumizi ya plastiki.

Akiongea katika tukio hilo Mhe. Jafo alisema kuwa suala la usafi katika fukwe ni la muhimu sana kwani ni sehemu ambayo watu huenda kwa ajili ya kujipumzisha hivyo ni lazima sehemu hizo ziwe safi muda wote.

"Fukwe ni sehemu ya Wananchi kupumzika mtu ukiwa na msongo wa mawazo ukija fukweni ukiangalia maji moyo unapata amani hivyo basi ni lazima tuhakikishe tunazitunza fukwe zetu kwa kuhakikisha mazingira yote ya mahali hapa yanakua safi na salama".

Vilevile Waziri Dkt. Jafo alisisitiza kwa Taasisi zote za Serikali kutilia mkazo matumizi ya nishati mbadala na kuacha kutumia mkaa au kuni. Amesema tukitumia nishati mbadala tunapunguza matumizi ya kuni na mkaa.

"Niziagize Taasisi zote za Serikali kama vile Majeshi ikiwemo Magereza, Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Vyuo vyote pamoja na Shule zote za Sekondari na Msingi (Binafsi na Serikali) kuanza kutumia nishati mbadala na majiko banifu. Nimewaomba STAMICO ambao wameanza kutengeneza mkaa badala ya kutumia makaa ya mawe kuongeza uzalishaji zaidi ili kuweza kutimiza mahitaji ya Wananchi wengi."

Aidha kwa upande mwingine pia Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mh. Dkt Selemani Jafo alizindua kampeni hiyo ya ***zero plastic*** kwa kuhamasisha wananchi kutumia vifaa mbalimbali vinavyotengenezwa kwa kutumia miti ya mianzi kama vile miswaki, vikombe na mirija ya kunywea vinywaji mbalimbali. Vifaa hivyo vilikua vikionyeshwa katika uzinduzi huo ambapo Wananchi wamepata fursa ya kuviona na kujifunza.

Naye Balozi wa Mazingira aliyeandaa kampeni hiyo ya zero plastic Laura Kivuyo ameishukuru Serikali kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za Vijana katika suala zima la utunzaji na Uhifadhi wa Mazingira na kuhamasisha jamii kuendelea kutunza na kuhifadhi Mazingira.

makala

# NEMC YATEKELEZA AJENDA YA KIMATAIFA YA "MAENDELEO ENDELEVU YA MILIMA"



Asilimia 25% ya Dunia ni sehemu ya milima ambayo ina umuhimu mkubwa katika kuboresha na kurekebisha hali ya hewa, kwa mfano, kufyonza hewa ukaa na zaidi kuwa makazi ya viumbe hai mbalimbali. Umuhimu huo wa ikolojia ya milima ulitambulika na kudhihirika katika lengo la Umoja wa Mataifa la Maendeleo endelevu (Ajenda 11, 2030). Lengo hili litatambua kuwa: kwa maendeleo endelevu lazima tutambue umuhimu wa viashiria hatarishi kwa mifumo ya ikolojia ya milima na hatimaye juhudi za pamoja za kulinda na kuhifadhi milima. Vilevile katika lengo la 15.2 inahitajika ifikapo 2020 kuhakikisha uhifadhi, urejeshaji na ufanyaji matumizi endelevu ya ikolojia ya nchi kavu na majini na huduma zinazotolewa kama misitu, ardhi oevu, milima kulingana na majukumu yaliyopo chini ya makubaliano ya kimataifa. Pia lengo la 15.4 linataka kufikia mwaka 2030 kuhakikisha uhifadhi wa ikolojia ya milima ikihusisha bioanui ili kuipa uwezo wa kutoa huduma muhimu kwa maendeleo endelevu.

Tanzania ina milima yenye mifumo tata ya kikolojia, yenye muundo wa kipekee, kutoa huduma ya kiikolojia, kuwa na aina nyingi za viumbe hai, kuwa na rasilimali maji na madini na umhimu katika sekta ya utalii. Mfano mlima Kilimanjaro, milima ya Uluguru, milima ya uwanda wa Makonde, milima Matengo, milima Uporoto, milima ya Livingstones na milima Usambara. Kutokana na unyeti wa rasilimali ya milima hii, Tanzania ilisaini mikataba hiyo na kuwa miongoni mwa mwanachama wa Umoja wa Mataifa wa kutekeleza Ajenda ya Azimio la Umoja wa Mataifa (General Assembly Resolution A/RES/71/234) ya mwaka 2030 kuhusu Maendeleo Endelevu ya Milima. Ajenda hii inasimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, Baraza la Taifa la Hifadhi na Uasimamizi wa Mazingira (NEMC) ambaye ndiye mtekelezaji wa Ajenda hiyo kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004.

Hii ni kutokana na kuwepo kwa sababu mbalimbali za kiasili na za kibinadamu ambazo zinapelekea uharibifu wa mifumo ikolojia ya milima hiyo kama vile kuchoma moto hovyo, maporomoko ya ardhi na mmomonyoko wa udongo. Vilevile, mabadiliko ya matumizi ya ardhi, uwindaji, shughuli za uchimbaji madini, milipuko wa volkano, mafuriko na uondashaji wa uoto wa asili na udongo kutokana na kilimo kisichokuwa endelevu huchangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa milima. Shughuli hizi mara nyingi husababishwa na kilimo cha mazao ya chakula, biashara na misitu, mifugo na viwanda vya uziduaji. Hivyo kuna umhimu wa kuingia makubaliano ya Kimataifa ili kuweza kuwa na mkakati maalumu wa kuyalinda na kuyahidhi maeneo hayo ili kuondoa au kupunguza athari hasi zinazoyakabili maeneo hayo.

Kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Baraza limekua likianisha maeneo ya vilima na milima yaliyopo Tanzania ambayo yapo katika hali hatarishi ya kuharibiwa. Katika uainishaji maeneo hayo, Baraza limekuwa likifanya tathmini ya mifumo ikolojia ya maeneo hayo mara kwa mara ili kuweza kuona uwezekano wa kuyahifadhi kwa kutumia zana ya Milenia kwa muda

Inaendelea Uk. 07

# JAFO AHIMIZA UTUNZAJI NA UHIFADHI WA MAZINGIRA - KISARAWE



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt Selemani Jafo akiwa ameshika mche wa mti kwa ajili ya kuupanda katika Msitu wa Kazimzumbwi wilayani Kisarawe mkoani Pwani*

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt. Seleman Jafo alihimiza utunzaji na uhifadhi wa Mazingira katika maeneo ya shule kama ajenda ya kudumu ya Kitaifa kwa kupanda mti shule ya Sekondari Janguo iliyopo Kata ya Msanga Wilaya ya Kisarawe Mkoa wa Pwani ili kuleta mandhari rafiki na yenye hewa safi kwa wanafunzi kusoma.

Zoezi hilo lilikuja mara baada ya kuhutubia wananchi, wazazi na wanafunzi wa shule hiyo katika mahafali ya 17 ya kidato cha nne yaliyofanyika shuleni hapo kwa kusisitiza umuhimu wa elimu pamoja na elimu ya mazingira kwani ndio msingi wa maendeleo endelevu katika jamii inayostawi.

Mhe. Jafo alisema elimu ya mazingira ni zaidi ya elimu nyingine yeyote inayompasa mtoto kuhimizwa, kufundishwa na kuelezwa tangu umri mdogo ili akue nayo hata atakapokuwa mzee kwani mazingira ni Uhai na ni afya.

"Ajenda ya upandaji miti ni ajenda ya kudumu ni ajenda ya Kitaifa, sasa hivi dunia inakabiliwa na changamoto kubwa ya mazingira, ukataji miti umeshamiri sana, tatizo la ukame limekuwa kubwa, tuilinde misitu yetu, niwaombe wakuu wa shule kote Nchini wasimamie ajenda ya soma na mti, kila mwanafunzi lazima apande mti, kwa ajili ya kutunza mazingira, Ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, hivyo kila Halmashauri inatakiwa kupanda miti milioni 1.5 Ili kufikia lengo la Kitaifa la upandaji miti milioni 276 kwa mwaka Nchi iwe ya kijani." Amesisitiza Mhe.Dkt. Jafo

Pamoja na kupanda mti, Mhe.Jafo pia alitembelea klabu ya kupinga rushwa, elimu inayotolewa shuleni hapo.



Inatoka Uk. 05

makala

# NEMC YATEKELEZA AGENDA YA KIMATAIFA ...





*Wataalmu wa NEMC wakiwa katika mlima Nyanzanga kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo ya jinsi ya kutumia mfumo mpya tathmini ya ikolojia ya milima.*

wa miongo miwili toka ianzishwe na Umoja wa Mataifa mwanzoni mwa mwaka 2000. Zana hii ilionekana kuwa na mapungufu kadhaa kwa kuwa haiakisi uhalisia wa eneo husika na kusababisha changamoto katika muundo wa tathmini, ukusanyaji wa taarifa, uandishi wa ripoti na ugumu katika kuhifadhi taarifa. Sababu hii imepelekea umuhimu wa kuwa na zana ya kufanya tathimini ya ikolojia ya Milima itakayoakisi uhalisia wa maeneo na kutoa maana halisi ya milima iliyoko na mipaka ya tathmini ili kuakisi mahitaji ya Sheria ya Mazingira Cap 191 ya mwaka 2004.


Kutokana na changamoto hizo, mwaka 2020 NEMC kupitia Kurugenzi ya Tafiti ya Mazingira iliandaa semina iliyojumuisha wataalamu mbalimbali kutoka katika Taasisi za Serikali, Idara, Mashirika, watafiti na wanafunzi wa vyuo vikuu ili kwa pamoja kujadili kwa upana na kuja na ripoti inayoonyesha mfumo mpya wa Tathmini ya Ikolojia ya Milima kuakisi uhalisia wa Tanzanzia Julai 5, 2020. Hatimaye Baraza limetoa ripoti ya namna mfumo huo uatakavyofanya kazi. Kwa awamu ya kwanza mwaka 2000, NEMC ilipima uwezo wa zana yenye mfumo mpya unaoakisi eneo husika kwa kufanya tathmini ya ikolojia ya milima ili kupima ufanisi na wake na kuthibitisha matumizi yake katika Mikoa ya Dodoma na Iringa.

Aidha kwa sasa Baraza limeshafanya mafunzo kwa ajili ya kuwajengea uelewa juu ya zana inayotumia mfumo mpya wa kufanya tathmini ya mfumo ikolojia ya milima (Framework and its accessories mobile app KOBO TOOLBOX) kwa Maafisa wa NEMC na viongozi wa Serikali za Mitaa katika Mikoa ya Mwanza, Iringa, Mbeya, Songwe na Njombe. Pia Baraza limeshanya majaribio ya kufanya Tathmini ya mifumo ikolojia ya milima ya Nyanzaga, Imezu na kilima cha Sweko kilichopo Mkoa wa Iringa

Zana ya kufanya Tathmini ya mifumo ikolojia wa milima imeonekana ni rahisi kuitumia na inaakisi uhalisia wa maeneo ya Tanzania haali ambayo inasaidai kupata taarifa sasa kutokana na eneo husika.



# WAZIRI JAFO ATOA SIKU TANO KWA KIKOSI KAZI CHA KUSIMAMIA MUONGOZO WA USAFISHAJI WA MCHANGA CHA MKOA WA DAR ES SALAAM




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais- Muungano na Mazingira Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kufanya ziara ya kutembelea Mto Msimbazi kata ya Mogo mtaa wa Kipawa, Jijini Dar es Salaam.*

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo alitoa muda wa siku nne kwa Kikosi kazi cha kusimamia Muongozo wa usafishaji mchanga kwa Mkoa wa Dar es Salaam kumpelekea taarifa ya nini kifanyike kuhusiana na kutafuta suluhisho na kupata ufumbuzi juu ya athari zinazotokana na uchimbaji wa mchanga katika Mto Msimbazi.

Aliyasema hayo alipokua katika ziara ya kutembelea Mto Msimbazi katika Kata ya Mogo Mtaa wa Kipawa katika jiji la Ilala Mkoani Dar es Salaam.

"Nimekuja hapa sababu Ofisi yangu imepokea malalamiko kuhusiana na athari za kimazingira zinazotokana na suala zima la usafishaji wa mto huu wa Msimbazi. Na kwa sababu kuna mawazo kinzani kutoka kwa pande mbili. Ninawapa siku tano mjadiliane kwa kina nini kifanyike na mniletee taarifa hiyo Ofisini kwangu".

Aidha aliongeza kuwa baada ya kufika katika eneo hilo la Mto huo amesikiliza maoni ya Wananchi na amepata maoni yanayokinzana kwani wengine wanasema baada ya shughuli za usafishaji mto huo kuanza zimeleta athari kwa mazingira na wengine wamesema baada ya shughuli hizo kuanza usafishaji umeleta manufaa makubwa kwa jamii inayozunguka eneo hilo.

Akiongea baada ya maelekez o hayo Mkuu wa Wilaya wa Manispaa ya Ilala Mheshimiwa Ng'wilabuzu Ludigija alimuhakikishia Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais- Muungano na Mazingira Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo kuwa amepokea maelekezo hayo na watayafanyia kazi na kuyasimamia kwa karibu sana.

Naye Meneja wa NEMC Kanda ya Masharikі- Kaskazini Bwana Arnold Mapinduzi alisema kuwa Muongozo wa usafishaji mchanga umeelekeza suala hilo lifanyike kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa ikiwa ni pamoja wote wanaotaka kujishughulisha na suala hilo waombe vibali kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Bonde la Wami Ruvu.

makala

# GEREJI BUBU KERO KWA WANACHI NA CHANZO KIKUBWA CHA UCHAFUZI WA MAZINGIRA NCHINI

Tanzania kama zilivyo nchi nyingine duniani, inayo sifa ya kipekee katika suala la Mazingira hasa ikizingatiwa maudhui na mantiki yake inamgusa kila mtanzania kwa namna tofauti katika usimamiaji wake.

Katika Serikali ya awamu ya sita ya Mhe. Samia Suluhu Hassan yenye azma ya kumjali kila mwananchi kwa falsafa ya "Kazi iendelee" nguvu zaidi na mkazo mkubwa kupitia Baraza la Taifa la Uhifadhi na Utunzaji wa Mazingira umetiliwa katika kuyatunza na kuhifadhi ili kwa pamoja tuweze kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza kubwa likiwa mabadiliko ya Tabianchi.

Lakini kwa nchi ya Tanzania yapo maeneo mengi ambayo suala zima la mazingira linaathriwa sana na linaendelea kushamiri kwa kuwepo kwa gereji zisizorasmi (gereji bubu) kwenye makazi ya watu na pembezoni mwa barabara.

Kwa mfano: Katika Mkoa wa Dar es salaam ambao una Halmashauri tano ikiwemo Ilala, Temeke, Kinondoni, Ubungo na Kigamboni zimeshamiri kwa kuwa na gereji bubu hali ambayo suala la uchafuzi wa mazingira na kelele kwenye makazi ya watu limekuwa haliepukiki. Katika maeneo ya Magomeni, Tandale, Manzese, Kimara, Sinza kwa uchache wake utagundua sheria za Mipangomiji hazikuzingatiwa hali inayowatesa watu viumbe na mazingira kwa ujumla kwani uoto wa asili umeingiliwa na kuharibiwa.




Athari ya kwanza inayosababishwa na gereji bubu katika mazingira ni kelele. Kelele hizi zinazoletwa na shughuli za utengenezaji wa magari zimekuwa zikisumbua wananchi wanaoishi maeneo ya karibu na kupelekea madhara ya kiafya kwa wananchi. kupunguzwa kwa shughuli za akili, kuwepo kwa ugonjwa wa moyo, kuwashwa pamoja na kizuizi cha kinga kupungua na magonjwa mengine kuongezeka kwakasi. Hali hii hudumaza maendeleo na kudhoofisha afya za wakazi na ustawi kwa ujumla.

Athari nyingine ni uharibifu wa ikolojia ya ardhi na uoto wa asili unaoleta uharibifu wa mimea katika kukua na viumbe hai kukosa chakula katika maeneo hayo hasa pale zinapotumika kemikali katika utengenezaji wa magari hayo au upakaji wa rangi hasa ikizingatiwa hakuna utaalamu wa kutosha wa kufanya jambo hili ndivyo athari zinavyozidi kuwa kubwa zaidi.

Kadhalika gereji hizo zimekuwa chanzo kikubwa cha uchafuzi wa hali ya hewa kinachotokana na ufokaji wa moshi unaosababishwa wa magari mabovu au yanapofanyiwa huduma (service). Hii ni Pamoja na rangi zinazopakwa kwenye magari hali inayosababisha athari kwa mwanadamu ikiwepo matatizo ya upumuaji, mapafu pamoja na athari katika mabadiliko ya tabianchi.

Cheche za moto zinazotoka au kuruka wakati wa kuchomelea au kugonga vyuma pia huleta athari kwa mazingira kwani huua viumbe hai na kuharibu pia ikolojia ya ardhi inayoleta uoto hasi wa asili na kusababisha mimea na ardhi kukosa rurtuba.

Ni dhahiri kabisa kwamba upo umuhimu wa wananchi wa Tanzania kujengewa uwezo wa kutambua sheria na masuala ya mazingira ili kuweza kuwa mstari wa mbele kuzuia au kutoa taarifa mahali popote au eneo lolote panapokuwa na dalili ya kuanzishwa kwa gereji bubu ili kuepukana na athari zinazoweza kujitokeza.

Ni muhimu kwa Halmashauri za miji na Manispaa kupitia idara za mipangomiji kutoa elimu kwa wajasiriamali na wananchi kwa ujumla wa namna sahihi ya uanzishwaji wa shughuli za kibinadamu kwa kuzingatia Sheria ya Mipangomiji katika maeneo ya makazi.

Vilevile, Serikali kupitia Halmashauri zake itenge maeneo ya pembezoni mwa Miji kwa ajili ya shughuli muhimu kama uendeshaji wa kumbi, Baa, gereji bubu na show rooms ili kuepukana na uchafuzi wa mazingira pamoja na usumbufu kwa wanadamu na mali zao.

makala

# ATHARI ZA UCHIMBAJI MADINI KWENYE MAZINGIRA

Madini ni malighafi inayopatikana duniani kiasili na huwa na tabia maalumu ya kikemia, mara nyingi huwa na (kristali) na huwa na rangi mbalimbali. Madini yapo takribani 4000 yaliyogunduliwa duniani na yapo kila mahali katika mazingira yetu. Tanzania ni nchi iliyobarikiwa kuwa na madini aina mbalimbali ambayo hupatikana katika baadhi ya mikoa ya Geita, Arusha, Mbeya, Mwanza, Mara na Shinyanga. Mfano wa madini haya ni; Tanzanaiti, Almasi, Feruzi, Yakuti, Shaba, Dhahabu na Zumaridi.

Madini ni muhimu sana katika nchi yetu, uchumi wa madini nchini Tanzania kwa kiasi kikubwa unatokana na madini ya dhahabu, ambayo huchangia takribani asilimia 80 ya mapato yatokanayo na rasilimali kuendelea kuwa tulivu kwa mwaka 2022. Hata hivyo, shughuli za uchimbaji wa madini zimekuwa chanzo cha uharibifu kwenye mazingira.

Maeneo yaliyokaribu na migodi yanaathiriwa na mmomonyoko wa kwenye miteremko iliyowazi na mabwawa ya mikia ambayo husababisha kujaa kwa mifereji na mito. Mfumo ikolojia wa mimea huathirika kutokana na mmomonyoko wa udongo ambao hupunguza maji yanayopatikana kwa ukuaji wa mimea.

Katika shughuli za uchimbaji wa madini, kuna uchafuzi wa hewa ambayo ni mojawapo ya athari zitokanazo na uchimbaji wa madini kwenye mazingira. Athari hizi husababishwa wakati mamia ya miamba yanapochimbwa, kukatwa na kusagwa na hivyo kuongeza kwa kiasi kikubwa kiwango cha vumbi hewani. Mikia ya migodi ambayo inaweza kuwa na taka iliyosagwa vizuri na hata yenye sumu inaweza pia kutawanyika angani.

Mifereji ya miamba ya asidi hutokea kiasili katika baadhi ya mazingira haya kama matokeo ya hali ya hewa ya miamba, lakini inafanywa kuwa mbaya zaidi na usumbufu mkubwa wa ardhi unaosababishwa na uchimbaji madini. Mifereji ya maji yenye asidi ambayo inaweza kuchoma ngozi ya binadamu na kuua samaki na viumbe vya majini inaweza kuwa na tindikali mara 20 hadi 300 zaidi ya mvua ya asidi.

Aidha ukataji wa miti unaosababishwa na uchimbaji wa madini unaweza kudhuru misitu iliyo karibu na makazi ya wanyama pori, kusababisha kutoweka kwa spishi. Vilevile ardhi ya kilimo inaharibiwa wakati miti, mimea na udongo wa juu vinapoondolewa kwenye eneo la migodi na kuathiri uzalishaji wa chakula. Uchimbaji madini lazima ufuate sheria zilizopo za kuhifadhi na kutunza mazingira. Hii uepusha uchimbaji haramu unachangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa misitu.

Vilevile athari kwa baoanuwai ni mojawapo ya athari za uchimbaji madini kwenye mazingira. Usumbufu mwingine ni kama vile, sumu ya taka ya mgodi kwenye mifumo ikolojia ambayo hutokea kwa kiwango kikubwa kuliko maeneo ya unyonyaji. Kupandikizwa kwa mgodi kunawakilisha mabadiliko makubwa ya makazi. Matoleo ya nyenzo za kazi za kibinadamu "anthropogenic activities" na uharibifu utokanao na mabadiliko makubwa yanaweza kuwa na athari kubwa kwa bioanuwai ya ndani.

Kuna athari za uchimbaji wa madini kwenye mazingira ambazo haziwezi kuepukika hivyo basi, kuna haja ya kutengeneza mpango wa kuhakikisha athari zake zinapunguzwa makali kwa kusaidiana na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC). Ili kufuatilia jinsi gani mapendekezo hayo yanafanyiwa kazi ni muhimu sana kufanya ufuatiliaji na kutoa elimu kwa wadau mbalimbali hasa wanaohusika na uchimbaji madini kuhakikisha mazingira yanatunzwa wakati wa shughuli za uchimbaji wa madini.



# TANZANIA YASHIRIKI MKUTANO WA UMOJA WA MATAIFA WA MABADILIKO YA TABIANCHI



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akiwa katika picha ya pamoja na wageni mbalimbali waliotembelea banda la maonesho la Tanzania katika Mkutano wa 27 wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi unliofanyika Novemba 2022, Sharm El- Sheikh nchini Misri.*

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mhe.Dkt.Selemani Jafo amekutana na waandishi wa habari juu ya ushiriki wa Tanzania katika mkutano wa wanachama wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi utakaofanyika tarehe 7-8 Novemba 2022 Sharm El- Sheikh nchini Misri.

Mkutano huo utahudhuriwa na wajumbe takribani 35000 kutoka nchi mbalimbali Duniani wakiwemo wakuu wa Nchi na serikali, Mawaziri na wataalamu waliobobea katika masuala ya mabaliko ya tabianchi.

Waziri Jafo amethibitisha ushiriki wa Tanzania katika mkutano na kuongeza kuwa Tanzania imedhamiria kushiriki kitofauti na miaka ya nyuma katika mikutano iliuopita kwa kuandaa banda la maonesho ambalo litakuwa na shughuli na maonesho ya kazi za kuitangaza nchi yetu.

Aidha Dkt.Jafo amesema" Tanzania itashiriki kikamilifu katika majadiliano ya masuala yenye maslahi mapana kwa Nchi yetu na kuweka msimamo katika uhimilivu wa mabadiliko ya Tabiachi, upunguzaji gesi joto na masoko ya kaboni na mbinu zisizo za masoko ili kukabiliana au kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi" ili kutangaza utalii wa Tanzania na kuhifadhi mazingira yetu.



*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) Bw. Abdallah Hassan Mitawi akizungumza na baadhi ya wageni waliotembelea banda la maonesho la Tanzania katika Mkutano huo.*

# NAFASI YA MAENEO YA BINADAMU NA HIFADHI HAI KATIKA KUHIFADHI MAZINGIRA

Uhifadhi wa mazingira ni mhimili muhimu katika kuhakikisha kuwa raslimali asilia zinatumika kwa njia endelevu. Ili kuwezesha matumizi hayo endelevu yanazingatiwa, imewekwa mikakati ya kitaifa na kimataifa. Andiko hili litaangazia zaidi programu ya kimataifa iliyoanzishwa mwaka 1970 chini ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) ambayo inayatambua maeneo mbalimbali kwa kuyajumuisha kwenye mtandao wa Dunia wa Binadamu na Hifadhi Hai (World Network of Biosphere Reserves).. Maeneo ya Binadamu na Hifadhi Hai yanaweza kuwa maeneo ya mifumo ikolojia ya nchi kavu, bahari au vyote kwa pamoja.

Lakini dhana ya "binadamu na hifadhi hai" ni nini? Ili kujibu swali hili kikamilifu, ni muhimu kwanza kutazama mfumo ambao umeendelea kutumika katika kuhifadhi mazingira na raslimali nyingine asilia. Kwa muda mrefu nchi nyingi duniani zimekuwa zikitenga maeneo kama vile hifadhi za wanyama pori, maeneo oevu, misitu na maeneo ya kihistoria kwa kuyawekea sheria ambazo zinatenganisha au kuweka mipaka kuzuia shughuli za kibinadamu zisifanyike ndani ya maeneo hayo. Hata hivyo, mfumo huo umeendelea kukumbana na changamoto mbalimbali ikiwemo binadamu kuyaingilia maeneo hayo lindwa au kutumia rasilimali husika kinyume cha sheria. Hii inatokana zaidi na shughuli za kibinadamu zinazoongezeka sambamba na ongezeko la idadi ya watu duniani. Dhana hii inazingatia mambo makuu matatu (3) ambayo ni: Uhifadhi; Maendeleo; na Elimu na Utafiti.

Kwa muktadha huo, Programu ya Binadamu na Hifadhi Hai chini ya UNESCO, inakuja na dhana au mfumo ambao unaweka misingi ya kuzingatia uhifadhi wa mazingira na rasilimali nyingine asilia bila kuzuia shughuli za kibinadamu. Hivyo, programu hiyo huoanisha dhana za shughuli za biandamu na ile ya uhifadhi ili vifanyike kwa pamoja katika mazingira yale yale. Mfano, programu hiyo ya UNESCO ilipoyatambua maeneo ya Misitu ya Usambara Mashariki kama eneo la Binadamu na Hifadhi Hai mwaka 2000, ilijumuisha miradi mbalimbali ikiwemo ule wa kuhaulisha taka ngumu kuwa nishati ya kupikia kama mbadala wa kuni. Kwa kuanzisha mradi huo, wakazi waliopo pembezoni mwa misitu ya Usambara Mashariki walipata nishati mbadala hivyo kupunguza au kuacha kabisa kukata miti kwenye misitu hiyo kwa ajili ya kuni. Kwa mantiki hiyo, dhana tajwa inalenga kumuwezesha binadamu kuishi na rasilimali asilia bila kuziharibu huku shughuli zake zikiendelea kama kawaida. Kupitia dhana hii Binadamu anahusishwa kwa karibu zaidi katika usimamizi na matumizi endelevu ya mazingira na rasimali zilizopo.

### Mambo ya Kuzingatia Katika Uteuzi wa Maeneo ya Binadamu na Hifadhi Hai

Uteuzi wa Maeneo ya Binadamu na Hifadhi Hai unazigatia taratibu mbalimbali kama ifuatavyo;

a) Kuwepo maeneo ya kanda (zonation)
b) Kuwepo kwa mifumo ya usimamizi (management regime)
c) Kuwepo na ushirikishwaji wa wadau katika ngazi zote
d) kutokuwepo kwa migogoro ya ardhi au mipaka
e) Kuwepo kwa mpango wa usimamizi wa Hifadhi Hai (management plan)
f) Sahihi za viongozi kutoka maeneo na taasisi husika za usimamizi
g) Uharibifu wa maeneo mengine ya kati na ya nje (buffer na transition zones)
h) Lazima kutumia "Muundo wa Kisheria wa UNESCO "UNESCO Statutory Frameworks (Seville strategy, Madrid Action Plan and Nomination Forms)
i) Lazima pia kutumia "Muundo wa Kisheria wa nchi husika (EMA 2004, NERA n.k.) na Taasisi zinazotumia sheria hizo
j) Eneo kupendekezwa na nchi husika kupitia Kamati ya Kitaifa ya Binadamu na Hifadhi Hai (National MAB Committee).

### Mpangilio wa Maeneo ya Kanda katika Hifadhi Hai

Mfumo wa Programu ya Binadamu na Hifadhi Hai chini ya UNESCO unaweka misingi ya uendeshaji wa maeneo yaliyoteuliwa kuwa Hifadhi Hai katika kanda mbalimbali za matumizi. Mfumo huo ni kama inavyoonekana katika Picha ifuatayo:

### Faida zinazotokana na Hifadhi Hai


Faida zinazotokana na Hifadhi Hai ni pamoja na;

a) Kufahamika na/au kujitangaza kimataifa kupitia mtandao wa dunia wa Hifadhi Hai;
b) Ushiriki kwenye mtandao wa dunia wa binadamu na hifadhi hai katika kubadilishana taarifa, uzoefu na ujuzi;
c) Maeneo muhimu kwa maendeleo ikiwa ni pamoja na uchumi wa bluu;
d) Hifadhi Hai kutumika kama maeneo darasa kwa kufanya mafunzo na majaribio, na kukusanya taarifa mbalimbali kuhusiana na hifadhi ya bioanuai na maendeleo endelevu;
e) Maeneo ya tafiti na kuandikia miradi; na
f) Kutumika kama mpango wa matumizi bora ya ardhi – (management tool).
g) Kusaidia katika kupunguza migongano (conflict management)
h) Wananchi kuwa sehemu ya usimamizi wa rasilimali asilia

### Hifadhi Hai Tanzania

Hadi kufikia mwaka 2022, Tanzania, kupitia Kamati ya Kitaifa ya Binadamu na Hifadhi Hai (National MAB Committee) inayo maeneo matano ambayo yameshajumuishwa kwenye Mtandao wa Kidunia wa Hifadhi Hai (World Network of Biosphere Reserves) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO). Maoneo hayo ni;

a) Hifadhi Hai ya Ziwa Manyara (iliyojumuishwa mwaka 1981)
b) Hifadhi Hai ya Serengeti-Ngorongoro (iliyojumuishwa mwaka 1981)
c) Hifadhi Hai ya Usambara Mashariki (iliyojumuishwa mwaka 2000)
d) Hifadhi Hai ya Jozani Ghuba ya Chwaka (iliyojumuishwa mwaka 2016)
e) Hifadhi Hai ya Gombe-Masito-Ugalla (iliyojumuishwa mwaka 2018)




**Picha Na. 1:** *Mpangilio wa Maeneo ya Kanda*

Inaendelea Uk. 014 >>

# WAZIRI JAFO ASHIRIKI ZOEZI LA KUPANDA MITI KATIKA WILAYA YA BAGAMOYO




*Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Dk. Seleman Jaffo (katikati), akiwa na wanafunzi wa Shule ya Msingi Mtoni, Wilaya ya Bagamoyo Mkoa wa Pwani wakati wa zoezi la upandaji miti Wilayani humo.*

Waziri wa Nchi ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt Selemani Jafo alishiriki katika zoezi la upandaji miti lililofanyika katika shule ya Msingi Mtoni iliyopo katika Wilaya ya Bagamoyo.

Akiwa shuleni hapo alipongeza Benki ya Standard Chattered ambao ndiyo waandaaji na wasimamizi wakubwa wa tukio hilo la upandaji miti katika shule hiyo.

"Nawapongeza sana benki ya Standard Chattered kwa kunialika kuwa Mgeni Rasmi katika shughuli hii ya upandaji miti ambayo ni mwendellezo wa juhudi katika kuendelea kutunza na kuhifadhi mazingira kwa kupanda miti"

Aidha ameziagiza Halmashauri zote Nchini ambazo hazijafikia malengo ya upandaji miti kama ilivyokua imeelekezwa awali kuhakikisha wanapanda miti na kufanikisha azma hiyo ya Serikali ya ukupanda miti kwa wingi katika kila Halmashauri Nchini ili kuweza kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

**"Naagiza Halmashauri zote kuhakikisha zinafikia malengo ya kupanda miti ili kuweza kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Mabadiliko ya tabianchi ni changamoto kubwa inayoikabili dunia kwani husababisha, ukame, kuongezeka kwa kina cha bahari na maziwa"**

Naye Mkurugenzi wa Standard Chattered Bwana Herman Kasekende alisema watendelea kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kusimamia zoezi la upandaji miti katika mashule mbalimbali ili kusaidia kutunza na kuhifadhi mazingira.

Inatoka Uk. 012

makala

# NAFASI YA MAENEO YA BINADAMU NA ...




**Ramani Na. 1:** *Hifadhi Hai Nchini Tanzania hadi kufikia mwaka 2022*

Hifadhi Hai Pendekezwa ya Rufiji-Mafia-Kibiti-Kilwa (RUMAKI)

Tanzania inatarajia kuwa na eneo la sita litakalojumuishwa kwenye Mtandao wa Dunia wa Hifadhi Hai chini ya UNESCO hivi karibuni. Eneo hilo ni lile la Rufiji-Mafia-Kibiti-Kilwa (RUMAKI) linalojumuisha mifumo ikolojia ya bahari na nchi kavu katika Wilaya za Rufiji, Mafia, Kibiti na Kilwa. Kwa muda mrefu, eneo hili limekuwa likihifadhiwa na serikali (chini ya Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu-MPRU, Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia-MIMP, Wakala wa Misitu Tanzania-TFS) na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyama Pori Tanzania-TAWA) na kusaidiwa na mashirika mbalimbali mfano Wild Wide Fund for Nature (WWF) kuendeleza shughuli za utafiti, utalii na elimu.

Kwa kuendeleza juhudi hizi nzuri, Kamati ya Kitaifa ya Binadamu na Hifadhi Hai (National MAB Committee) kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ambalo ndilo linaloiratibu Kamati tajwa, ilikaa na kukubaliana kulipendekeza eneo la Rufiji-Mafia-Kilwa-Kibiti kuingia kwenye Mtandao wa Dunia wa Binadamu na Hifadhi Hai. Hii ni kutokana na eneo hilo kuwa na sifa zifuatazo;


a) Eneo la Msitu wa Mikoko la Rufiji ambalo linasimamiwa na Wakala wa Misitu (TFS).
b) Eneo la Hifadhi Tengefu ya Bahari ambayo linasimamiwa na Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU)
c) Eneo la Magofu ya Kilwa (Kilwa Ruins) chini ya TAWA
d) Maeneo ya usimamizi shirikishi jamii ya wavuvi: Beach Management Units (BMUs)
e) Maeneo ya ardhi oevu ya RUMAKI: Ramsar Site (IBA, nk)

Katika pendekezo la RUMAKI kujumuishwa kwenye Mtandao wa Kidunia wa Hifadhi Hai, Kamati ya Kitaifa ya Hifadhi hai imependekeza maeneo ya kikanda ndani ya RUMAKI kama ifuatavyo;

a) Eneo la Kitovu (ndani) (Core zone): Hili litajumuisha maeneo yaliyo ndani ya Hifadhi ya Bahari Mafia na maeneo tengefu matatu (Shungimbili, Nyororo na Mbarakuni); Misitu ya Hifadhi ya Mikoko-Ukanda 1; Misitu ya Hifadhi mwambao wa Pwani (Tamburu, Mto Muhoro, Mlola - Rufiji, Mafia, Kibiti, Kilwa); Hifadhi ya Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara-WHS
b) Eneo la Kati linalozunguka eneo la kitovu (Buffer Zone): Maeneo ya usimamizi shirikishi jamii ya wavuvi - CFMAs, Misitu ya uzalishaji - Kanda 2-4; Misitu ya mwambao wa Pwani (Mchungu, Kitope, Kikale na Muhoro)
c) Eneo la nje kabisa (Transition zone): Linajumuisha eneo la matumizi ya watu na shughuli zao (Rufiji, Mafia, Kibiti na Kilwa).


Taratibu zinazohusika ikiwemo ushirikishwaji wa wadau katika Wilaya zote nne umeshafanyika na ombi husika kuwasilishwa UNESCO Makao Makuu, Paris, Nchini Ufaransa. Aidha, Shirika hilo limeshatoa maoni ya awali kuhusu ombi hilo, ikiwemo kulitaka Baraza kuwasilisha ridhaa (saini mbalimbali) kutoka Wilaya ya Rufiji na Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU). Baraza limeshachukua hatua stahiki na kuziwasilisha saini hizo. Ombi hilo linaendelea kupitiwa na Tume ya Kimataifa ya Kuratibu Masuala ya Hifadhi Hai (MAB International Coordinating Council-MAB ICC) na linatarajiwa kuridhiwa ifikapo Mwezi Juni, 2023.

Kutokana na programu ya Hifadhi Hai kuwa na mihimili mikuu mitatu ya Uhifadhi; Maendeleo Endelevu; na Taaluma na Tafiti, umuhimu wake katika kuhifadhi mazingira unajinadi pale ambapo programu hiyo inashadadia uwepo wa uendelevu (sustainability) katika matumizi ya rasilimali. Hii inatengeneza mahusiano yenye uwiano (balanced relationship) kati ya binadamu na mifumo ikolojia, kwa kuhakikisha kuwa binadamu anapata mahitaji yake muhimu lakini uwepo wa rasilimali asilia kwa vizazi vijavyo unazingatiwa. Aidha, programu hiyo pia inaongeza ufanisi katika uhifadhi wa mazingira kwani unatoa fursa kwa mwanadamu kuwa mlinzi wa kwanza wa mazingira yanayomzunguka tofauti na mifumo mingine ambayo inategemea Zaidi Sheria ili kusimamia uhifadhi wa mazingira.




**Ramani Na. 2:**

*Ramani ya Tanzania ikionesha eneo la RUMAKI*




**Ramani Na. 3:**

*Maeneo ya Kanda ndani ya RUMAKI*

# MAGARI YA TAKA NI CHANZO CHA UCHAFUZI WA MAZINGIRA

Shughuli za binadamu ni kitu kisichoepukika toka kuumbwa kwa ulimwengu kwani ndiko kunakodhihirisha uzima wake.

Shughuli hizi zipo za aina mbalimbali, zikiwemo za kilimo, ufugaji, ujasiriamali, shughuli za nyumbani na nyingine nyingi.

Ufanyikaji wa shughuli hizi mwisho wake huzalisha malighafi mbalimbali ambazo nyingine zaweza kurejelezwa na nyingine haziwezi kurejelezwa na kugeuka kuwa taka zinazotakiwa kusafirishwa hadi kwenye madampo kwa kutumia magari ya kubebea taka.

Mara nyingi taka hizi hasa sehemu za mitaani hubebwa na magari yaliyochoka au mabovu kutokana na dhana potofu ya kwamba gari aina ya lori likishachoka ndio linapewa kazi ya kuzoa taka kutoka maeneo ya uzalishaji hadi kwenye eneo la kutupa zikiwemo kwenye viroba kutoka eneo moja kwenda jingine.

Dhana hii ni potofu kwani uchafu unahitajika kuhifadhiwa vizuri ili kulinda afya za wanadamu na kuepuka uchafu kuzagaa kwenye mazingira.

Makala hii imelenga kuzungumzia magari mabovu yanayobeba taka zinazozalishwa kutokana na shughuli za nyumbani na kutupwa maeneo yaliyotengwa na Serikali ya Mtaa au kijiji kwa ajili hiyo.

Magari aina ya malori yenye uwazi nyuma ambayo mengi yao ni mabovu yanatumiwa sana na vikundi maalumu vya mitaani kubeba taka hali inayoweza kuhatarisha usalama wa raia wanaowazunguka maeneo hayo pamoja na mali zao kwa kuchafuka kwa mazingira maeneo husika.

Mara nyingi taka za majumbani zinazozalishwa kutokana na shughuli za nyumbani zimegawanyika katika makundi ambayo uhifadhi wake unatakiwa kuzingatia aina ya taka. Kwa taka ngumu uhifadhi wake ni rahisi, lakini kwa taka za unyevunyevu kunahitajika umakini wa hali ya juu hali ambayo magari ya taka kutokana na ubovu wake uzingatiaji wa usalama na afya unakuwa mgumu. Hivyo basi hali hii husababisha kutiririka kwa maji pindi zinapokuwa kwenye magari wakati wa kusafirishwa hali inayochafua mazingira na wakati mwingine hata kuchangia magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu.

Magari hayo pia yanakosa vifaa muhimu vya kubebea taka hali inayosababisha uchafuzi wa hali ya hewa unaotokana na uchafu huo kutokufunikwa na kusababisha takataka kujaa sana na kumwagika wakati wa kupelekwa kwenye madampo ya mitaa.

Pia kulingana na tathmini za kitabibu, moshi unaofuka kwenye magari hayo pia huchafua hali ya hewa na kuathiri afya za binadamu hasa katika upumuaji na kupelekea matatizo makubwa kama pumu, TB na mengineyo mengi.

Magari hayo pia yamekuwa chanzo cha kelele mitaani kutokana na mngurumo wake kuwa mbovu na wenye sauti kubwa unaosababishwa na kutofanyiwa marekebisho 'service' kwa wakati, hali inayoweza kusababisha magonjwa ya vichwa, kushindwa kufikiri, magonjwa ya moyo pamoja na shinikizo la damu kulingana na taarifa za kitabibu.

Wakati mwingine kutokana na ubovu wa gari na pengine na barabara za Mitaani kutokuwa rafiki, magari haya hutelekezwa pembezoni mwa barabara yakiwa na takataka na kugeuzwa dampo hali ambayo sio afya.

Ni vema kutumia magari mazima kwa ajili ya kusafirisha taka kutoka sehemu moja hadi nyingine ili kuepuka kuchafua mazingira na kulinda usalama wa watu na afya zao.



makala

# UTUNZAJI NA UHIFADHI WA MAZINGIRA KATIKA UCHIMBAJI WA MADINI



Tunatambua kuwa kwa hali ya sasa utajiri mkubwa Nchini Tanzania unatokana na madini pia unatoa fursa kwa jamii yetu ikiwemo upatikanaji wa ajira kwa vijana na kuchangia ongezeko la kipato kwa Wananchi. Tunatambua kuwa sekta ya madini inamchango mkubwa sana katika jamii yetu lakini imekuwa inachagamoto kubwa katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira.

shughuli za uchimbaji zimegawanyika katika makundi mawili ambayo kuna wachimbaji wadogo na wachimbaji wakubwa, mara nyingi wachimbaji wakubwa wanajitahidi katika kusimamia mazingira na kuzingatia Sheria wakati wa utekelezaji wa shughuli zao, lakini changamoto kubwa ipo kwa wachimbaji wadogo ambao wanaangalia upatikanaji wa mali bila ya kuzingatia utunzaji wa mazingira na afya zao.

katika kupambana na utunzaji wa mazingira kwenye uchimbaji wa Madini Serikali kupitia Taasisi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) imeweza kusimamia kwa kiasi fulani japo changamoto ipo na bado Baraza linaendelea kutatua changamoto zilizopo ili kufikia lengo la Taifa katika uhifadhi wa mazingira.

Uchimbaji mdogo wa madini Tanzania ni moja ya kazi mbovu zenye athari kwa upande wa afya, usalama na mazingira. Imebainika kuwa wachimbaji wadogo wanafanya shughuli za uchimbaji bila ya kuwa na tahadhari za kiafya na kimazingira.

Geita, Mara na Shinyanga ni Mikoa iliyobarikiwa sana madini aina ya dhahabu ambako huko kuna wachimbaji wakubwa na wachimbaji wadogo wa dhahabu. Mikoa hii mitatu ni Mikoa ambayo inachangamoto kubwa katika usimamizi wa mazingira hususani katika miradi ya uchimbaji wa madini kwa wachimbaji wadogo. Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya 2004 katika migodi mikubwa ni rahisi tatizo kubwa lipo kwenye migodi ya wachimbaji wadogo ambao wanatumia tekinolojia dhaifu katika uchimbaji na kupelekea uharibifu wa mazingira na afya.

Kutokana na mamlaka iliyonayo Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limejitahidi kutoa elimu Mkoa wa Mara, Mwanza na Geita inayohusu mazingira kwa jamii inayojihusisha na shughuli za uchimbaji madini ikiwa ni pamoja na wamiliki wa mitambo ya kuchenjua dhahabu. elimu hii inatolewa kwa lengo la kukuza uelewa kwa wachimbaji wadoogo juu ya uzigatiaji wa Sheria ya Mazingira ya 2004.

Imebainika kuwa wachimbaji wadogo wa dhahabu hufanya kazi ya kuchimba madini bila ya kuzingatia Sheria ya Mazingira ya 2004, baada ya kupata kibali cha uchimbaji kutoka Wizara ya Madini hawafanyi Tathmini ya Athari kwa Mazingira kitu ambacho hakipo sahihi. Hivyo kutokana na chagamoto hiyo ndipo Baraza lilipoamua kutoa elimu ili kuweza kusaidia jamii hiyo kuwa na uelewa wa namna ya kulinda mazingira na kuzingatia Sheria.

Madini ni rasilimali asilia ambayo inachangia kipato katika Taifa na wananchi wake. wachimbaji wadogo wamekuwa wakichimba madini kujipatia kipato lakini wanafanya shughuli hizo bila ya kuzingatia utunzaji na uhifadhi wa mazingira. Changamoto kubwa iliyobainika kwa wachimbaji wadogo kutokana na ukaguzi uliofanywa na Baraza katika Mkoa wa Mara, Geita na shinyanga ikiwemo uchenjuaji wa dhahabu kwa kutumia kemikali aina ya zebaki.

Pamoja na kwamba elimu imekuwa ikitolewa mara kwa mara kuhusu madhara ya zebaki kwa wachimbaji wadogo lakini bado wachimbaji wadogo wengi hutumia kemikali hiyo katika kuchenjua dhahabu. Wachimbaji wadogo wengi hawachukui tahadhari badala ya kutumia kizuia mikono (gloves) kukinga mikono isidhurike kwa zebaki, wengi wao hutumia mikono na hapo ndipo zebaki inaweza kupenya kwenye ngozi na kuwaathiri.

Kemikali ya Zebaki kwa upande wa afya ya binadamu huathiri Mfumo wa Neva na kusababisha magonjwa kama miguu na mikono kufa ganzi na kukosa nguvu, misuli kulegea, figo kuathirika, uono hafifu, kupoteza uwezo wa kusikia na kuongea, mimba kuharibika, kuzaa watoto taahira au wenye viungo pungufu, kupoteza kumbukumbu, kukosa usingizi kwa muda mrefu, kiharusi na hatimaye kifo. Aidha magonjwa haya yanaweza kurithishwa kutoka kizazi hadi kizazi.

Zebaki kwenye mazingira inaathiri ubora wa hewa, udongo na pia vyanzo vya maji. Sumu kali ya zebaki inauwezo wa kuathiri samaki na viumbe wengine wa majini wanapokula sumu hiyo. Sumu ya zebaki inayo tabia ya kuongezeka makali kutoka inapoliwa na wadudu wadogo wa majini hadi inapoliwa na samaki wakubwa na hatimaye samaki hao wanapoliwa na binadamu. Hivyo, binadamu anapokula samaki ukali wa sumu ya zebaki unakuwa mara dufu na hatari sana kwa afya yake.

Kutokana na athari hizo Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuendelea kutoa elimu kwa umma hususani kwenye maeneo ya uchimbaji mdogo wa madini ya dhahabu kuhusu madhara ya zebaki na namna ya kujikinga ili kuepukana na madhara hayo na pia hatua za kuchukua ili kulinda mazingira yasiathirike na zebaki.

# IFAHAMU KWA UNDANI TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA (TAM)

Baraza la Taifa la Usimamizi na Hifadhi wa Mazingira lina kurugenzi tano za kiutendaji mojawapo ikiwa ni Kurugenzi ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira. Kurugenzi hii husimamia michakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kwa miradi mipya na taarifa za ukaguzi wa awali kwa miradi inayoendelea. Kurugenzi ya TAM husimamia kanzidata za miradi iliyosajiliwa kufanya TAM, miradi iliyosajiliwa kwa ukaguzi wa awali na taarifa za Wataalam Elekezi wa mazingira.

TAM ni mchakato unaotambulika duniani wa kufanya tathmini ya mazingira ili kubaini athari za mradi pendekezwa pindi utakapo anza utekelezaji wake. TAM inatoa fursa ya kubainisha namna ya kuzikabili athari zilizotambuliwa kwa kuzingatia faida na hasara za kijamii na mazingira. Utaratibu hu unawawezesha wasimamizi wa mazingira kufanya maamuzi yenye tija juu ya utekelezaji wa mradi. Vilevile, TAM husaidia kupatikana taarifa za mradi kwa kupitia maoni ya wadau mbalimbali na kupitia tafiti ili kuwezesha wataalam na wasimamizi wa mazingira kuanisha matatizo yanayoweza kujitokeza kama vile uchafuzi wa maji, ardhi na hewa, uharibu wa bionanui,kusitishwa shughuli za kiuchumi, jamii na utamaduni.

TAM ni nguzo muhimu katika kuhakikisha miradi endelevu nchini na yenye tija kwa taifa kwani husaidia kubainisha kwa kina faida na hasara za mradi; kuboresha usanifu wa mradi; kuelimisha na kutoa taarifa za mradi ili kuruhusu ushirikishwa wa jamii husika na kujenga mahusiano bora na wadau wa mradi; kuainisha mahitaji mna upatikananji wa raslimali zinatozatakiwa katika utekelezaji wa mradi; kusaidia kutunza kukmbukumbu za hali ya asili/iliyop katika eneo ambalo mradi, jamii inayozunguka na mazingira yaliyopo. Vilevile, TAM imekuwa ikitumiwa na taasisi za fedha kama nguzo muhimu ya maamuzi ya utoaji au kutokutoa fedha za utekelezaji wa mradi kwa kuzingatia jinsi gani athari za mradi zimetengenezewa mipango na mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo.

Mchakato wa TAM ni shirikishi wa wadau mbalimbali wanaoguswa na mradi na pia huhusisha wataalam wa kada mbalimbali. Athari zinazoainishwa katika mchakato wa TAM husaidia wataalam elekezi wa mazingira kutoa muongozo wa njia nzuri ya kukabiliana na athari hizo katika hatua zote za uendeshaji wa miradi ya maendeleo.Aidha, taarifa hiyo husaidia Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira kutoa mapendekezo kwa Waziri mwenye dhamana ya mazingira juu ya uidhinishaji wa utekelezaji wa mradi husika.

Pamoja na hatua hizo, miradi mingi ya maendeleo bado ina athari kadha wa kadha kwa mazingira kwani uendeshaji wake hutegemea ardhi na malighafi. Hali hiyo huchangia kumaliza rasilimali zinazotegemewa na jamii husika. Kwa mfano, hatua za maandalizi ya eneo la kutekeleza mradi huhusisha kufyeka au kukata mimea, hatua inayoweza kupelekea kupotea viumbe muhimu katika ikolojia. Wakati huo huo, usafirishaji wa vifaa vya ujenzi huleta usumbufu kwa jamii kwa kusababisha kelele na mitetemo.

Mbali na usumbufu huo, miradi ya maendeleo inaweza kupelekea mifarakano na jamii endapo maeneo yao yatachukuliwa, hali inayoweza kupelekea idadi kubwa ya watu kuhama na kuathiri muundo na utamaduni wa jamii. Aidha, athari za miradi ya maendeleo hudumu hata baada ya mradi kuacha kutelekezwa endapo mpango wa kusitisha mradi hautazingatia athari katika ardhi, maji ina hewa na kufanya jamii ishindwe kufanya shughuli zake za kijamii.

Baraza pia husimamia tathmini ya mazingira kwa miradi ambayo tayari inaendeshwa ili kubaini kiwango cha uhifadhi wa mazingira. Aidha, miradi inayoendeshwa hufanyiwa ukaguzi wa mazingira baada ya kupata cheti cha TAM ili Baraza liweze kutathmini kiwango cha utekelezaji wa masharti na ahadi za kulinda mazingira katika ripoti ya mazingira, na kwa miradi ambayo imeanza kufanya kazi kabla ya Kanuni ya TAM ya mwaka 2005.

Jamii inakumbushwa pia kuwa gharama za TAM zimegawanyika katika makundi mawili ikiwa ni pamoja na 1) Gharama za moja kwa moja za mradi; na 2) Gharama za mapitio ya mradi (ada za NEMC). Gharama za mradi zinategemea mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na1) mahitaji ya mradi ulipo (mfano eneo oevu, hifadhini, au kwenye chanzo cha maji); ukubwa wa mradi; aina ya mradi (mfano kiwanda cha dawa au sementi; jamii inayozunguka na mataraji yao. Gharama za moja kwa moja za TAM zinahusisha hatua zote za uaandaaji andiko. Gharama hizi zinajumuisha masuala mawili makubwa 1) Gharma za utaalam wa ufanyaji tathimini na uandaaji andiko na2) Gharama za upimaji, ufafiri, maladzi na ukusanyaji wa taarifa mbalimbali.

Tathmini ya Mazingira Kimkakati (TMK) inahusu tathmini ya athari kwa mazingira kwa sera, kanuni, mipango na programmu mbalimbali. Kama TAM, TMK hufanyika kabla ya sera, mikakakati na programu kuanza kufanya kazi. Tofauti ni kwamba TMK inahusu shughuli zenye ushawishi na athari pana kimaamuzi ambazo si za mradi mmoja mmoja kama ilivyo kwa TAM.

Michakato ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na ile ya ukaguzi wa mazingira inahusisha hatua mbalimbali ambapo taasisi na watu binafsi hutoa mawazo yao pia. Hivyo kabla ya

Inaendelea Uk. 018



Inatoka Uk. 017



# NAFASI IFAHAMU KWA UNDANI (TAM) ...

kuanza mchakato wa tathmini wa athari katika mazingira, mwekezaji anapaswa kutafuta mshauri muelekezi aliyesajiliwa na Baraza kupitia tovuti yetu www.nemc.or.tz, ili amsaidie katika mchakato huu kutokana na taaluma aliyonayo. Baraza husimamia mchakato wa tathmini kwa njia ya kielektroniki wa kusajili Miradi ya Tathmini za Mazingira na Ukaguzi, yaani, Online Registration and Tracking System kupitia https://eia.nemc.or.tz ambapo mwekezaji anaweza kusajili mradi wake na kuendelea na hatua tajwa hapo chini.

i. Muhtsari wa mradi: Mwekezaji akishirikiana na mtaalam mwelekezi, husajili mradi kwa kujaza fomu na kuwasilisha muhtasari wa mradi kwa ajili ya mapitio. Usajili huo huambatana na malipo ya Tshs. 200,000 ambazo hulipwa kwa kutumia mfumo wa malipo ya serikali baada ya kupata hati ya madai na kumbukumbu ya namba ya malipo. Baada ya kupokea maombi ya mwekezaji, Baraza huwatumia muhtasari wadau ili kupata maoni juu ya mradi na huchanganua muhtasari wa mradi ili kuanisha endapo utahitaji kufanyiwa tathmini ya kina au kuboresha muhtasari huo. Kiutaratibu, miradi yenye athari kubwa za mazingira huwa zinahitaji kufanya tathmini kina ya mazingira wakati ile ambayo haitarajiwi kuwa na athari kubwa, yaani kundi iliyo kwenye kundi B2 huishia kwenye muhtasari peke yake.

ii. Taarifa za awali na hadidu za rejea: Miradi inayohitaji TAM ya kina na ile iliyosajiliwa kwa ajili ya ukaguzi huwasilishwa na andiko la awali (scoping report) zenye kuainisha kwa ufupi taarifa zitakazo wekwa kwenye ripoti kubwa na hadidu za rejea zitakazotumika kukusanya taarifa hizo na kuandaa andiko. Katika hatua hii, mwekezaji anapaswa kuambatanisha uthibitisho wa kuwa wadau husika wamepokea taarifa za awali za mradi huo.

Baraza litampatia mwekezaji hati ya madai pamoja na kumbukumbu namba nyingine kwa ajili ya kulipia gharama za upitiaji wa ripoti ya TAM kama ilivyoainishwa katika kanuni ya Tozo na Ada ya mwaka 2021.

iii. TAM na Ukaguzi wa mazingira; Endapo Baraza litapitisha hadidu za rejea, mwekezaji atashirikiana na mshauri mwelekezi kufanya TAM kama ilivyoelekezwa katika kanuni ya 2005 na za 2018 za Tathmini ya athari ya mazingira.

iv. Taarifa ya TAM na Ugakuzi wa Mazingira: Taarifa zilizokusanywa huandaliwa na kuwasilishwa Baraza kwa ajili ya kupitiwa. Ili kujiridhisha na taarifa hizo, Baraza hufanya ukaguzi wa mradi na baada ya hapo, huwasilisha ripoti yake katika Kamati ya Ushauri ili kujadili mradi na kutoa mapendekezo kwa Baraza. Baada ya kikao cha Kamati, muhtasari huandaliwa pamoja na mapendekezo ambayo hupelekwa kwa mwekezaji kuboresha taarifa ya tathmini kwa kumshirikisha mshauri elekezi.

v. Cheti cha mazingira: Baada ya mwekezaji kuboresha taarifa zake, wataleta ripoti hio ilikuwezesha Baraza kuipitia tena na kuamua kumshauri Waziri kutoa cheti cha mazingira kwa mwekezaji au la. Endapo mradi utaidhinishwa na Waziri, mwekezaji atapatiwa cheti cha TAM.

vi. Masharti ya mradi: Baraza huandaa masharti ambayo muwekezaji anapaswa kuyazingatia wakati akitekeleza mradi wake. Baraza linaweza kugagua mradi huo ili kuthibitisha kama masharti hayo yanazingatiwa ikiwa ni pamoja na kutathmini iwapo mradi unazingatia Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004

Aidha, Sehemu ya nne ya Sheria ya Mazingira, 2004 imeweka misingi ya kufanya TAM na ukaguzi wa mazingira. Pamoja na Sheria ya Mazingira ya 2004, Kanuni ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira za mwaka 2018 na zile za mwaka 2005 zinamtaka mwekezaji kufanya TAM kwa miradi ya sekta mbalimbali ikiwemo migodi, viwanda, utalii na kilimo. Pamoja na taarifa ya TAM, Sheria na Kanuni zinatambua umihimu wa kushirikisha wadau husika wa mradi na hivyo humtaka mwekezaji kuwashirikisha kikamilifu.

Kanuni nyingine muhimu katika TAM ni Kanuni ya Usajili wa Wataalam Elekezi ya 2021 inayoainisha taratibu za kusajili Wataalam Waelekezi pamoja na majukumu yao na muongozo wa maadili ya kazi.

Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) ina faida nyingi ikiwa ni pamoja na kufanya maamuzi sahihi na yenye weledi juu ya utekelezaji wa mradi. Taarifa zinazotokona na TAM hupelekea watoa maamuzi kuwa na uelewa wa mradi na hivyo kufanya maamuzi sahihi na kupendekeza namna nzuri ya kuepusha athari hasi zinazoweza kujitokeza wakati wa utelekelezaji wa mradi husika. Ushirikishaji wa wadau na jamii katika mchakato wa TAM unaleta ufahamu juu ya mambo ya msingi ya mradi na kuchochea uwazi kwa kuhakikisha kwamba wadau wanatoa maoni yao kabla mradi hujaanza kutekelezwa. Pamoja na uwazi, ushirikishaji wa wadau kunasaidia mradi kukubalika mapema na kuondoa sitofahamu kwa jamii.

Ushirikishaji wa sekta nyingine kunamsaidia mwekezaji kujua matakwa ya sheria nyingine zinazoweza kuathiri uendeshaji wa mradi kama vile kupata kibali cha kutumia maji, kibali cha ujenzi na vingine pamoja na kuepuka gharam. Udhibiti wa athari za mradi kwa mazingira kabla ya utekelezaji husaidia kuokoa muda na gharama kwani athari nyingine zinaweza kufanyiwa kazi katika hatua ya usanifu kulingana na mapendekezo ya wataalamu pamoja na kuzingatia mbinu bora.

Pamoja na hayo, TAM inaweza kumsaidia mwekezaji kutokiuka Sheria na Kanuni, na gharama kubwa inayoweza kujitokeza kutokana na kusafisha mazingira yaliyochafuliwa au kuharibiwa kwa kufanya yafuatayo: Kusitisha mradi kwa njia salama, kwani mara nyingi miradi ya maendeleo inavyositishwa inahitaji kufuata taratibu za mazingira. Taratibu hizi huanishwa kama sehemu ya mpango wa kulinda na kusimamia mazingira kwenye TAM. Hivyo, mradi ukifika hatua ya kufungwa au kuacha kufanya kazi, mwekezaji ana jukumu la kuhakikisha kuwa anafanya jitihada za kurudisha eneo katika hali yake ya awali.

Vilevile pamoja na kuleta manufaa kwenye kutoa maamuzi na kusaidia maendeleo endelevu, zipo changamoto mbalimbali zinazotokana na mchakato kama ifuatavyo: 1) Utekelezaji mradi kabla kukamilisha mchakato wa TAM kinyume na matakwa ya Sheria, hali ambayo huathiri maamuzi ya mradi kwa uongozi, 2) Kutekeleza mradi kabla ya mchakato wa TAM unaweza kuleta changamoto kwa muwekezaji wakati wa kuomba vibali kwa mamlaka zinazohusika na mradi huo, na 3) Kutokushirikisha mshauri elekezi katika hatua za awali za mradi.

Kushirikisha mshauri mapema iwezekanavyo husaidia katika kuanisha athari za mradi kabla mradi haujasajiliwa, hivyo kumruhusu muwekezaji kuzingatia maswala muhimu katika utoaji wa cheti cha TAM kama vile mradi kuendana na matumizi ya ardhi na mipango ya kusimamia maeneo lindwa. Kuwasilisha taarifa za TAM na ukaguzi zilizo chini ya kiwango hali inayochangia kuchelewa kukamilika taratibu za TAM na Sera, Sheria, Kanuni na mipango kutokufanya TMK hivyo kupelekea changamoto katika kukamilisha TAM kwa miradi ambayo haikujumuishwa katika taratibu hizo. Hatua hiyo huchangia kudhorotesha uratibu wa kwa wadau kutoka sekta mbalimbali juu ya maswala ya mazingira kwa pamoja.







Kauli ya Mazingira Yetu















tu

ALHAMISI
25 AGOSTI,2022




na vifungashio vya viuatilifu ni
mu kuzirudisha chupa hizo katika
elezwa na kuzuia kusambaa kwa

## Kauli ya Mazingira Yetu

IJUMAA
08 JULAI, 2022



258

Sababu kubwa inayopelekea uharibifu wa hifadhi ya mikoko ni shughuli za kibinadamu zikiwemo kukata miti ya mikoko kwa ajili ya mbao na nguzo, kilimo cha chumvi na uvuvi wa kutumia kemikali. Tuepuke shughuli zinazochangia kuharibu mikoko.

tu


IJUMAA
22 JULAI, 2022



nibitiwa hutengeneza makorongo
a ya kilimo na kuyafanya yasiweze
mazingira ili kuepuka uharibifu wa

## Kauli ya Mazingira Yetu

JUMANNE
19 JULAI, 2022



13

Mojawapo ya athari za uharibifu wa mazingira ni kupungua kwa uwezo wa ardhi kuzalisha mazao. Hali hii inaweza kusababisha kuwepo kwa janga la njaa.

tu

JUMANNE
09 AGOSTI, 2022



gira ni upotevu wa rasilimali zake
ikolojia zinazotolewa na miti, hivyo
nazingira.

## Kauli ya Mazingira Yetu

ALHAMISI
14 JULAI ,2022



10

Idadi ya uchafu wa plastiki unaoingia kwenye mifumo ya ikolojia ya majini imeongezeka na inasababisha madhara makubwa kwa afya ya binadamu, uchumi duniani, bayoanuai na kwa hali ya hewa.

Kauli ya Mazingira Yetu

# KATUNI





















NOVEMBA 17, 2022
POOOH!
POOOH!
POOOH!
POOOOOH!
NDIO MAANA INASHAURIWA TUSIWEKE MAKAZI KARIBU NA BANDARI ILI KULINDA MAZINGIRA NA AFYA ZETU KUTOKANA NA KELELE
ENEO HILI LINA KELELE NYINGI



DISEMBA 20, 2022
ARDHI YETU IMEKUWA KAME KILA TUNAPOCHIMBA PAKAVU, NILIKUJA ILI UNIAZIME MAJI JAPO KIDOGO
MIMI PIA SINA MAJI HATA TONE, WANANGU WALIENDA UMBALI MREFU KUTAYAFUTA NA WAMEKOSA, CHANZO NI WANAOHARIBU MAZINGIRA, JAMII YETU LAZIMA ICHUKUE HATUA


NAONA UKAME MKALI UNATUNYEMELEA
CHANZO CHA YOTE NI BINADAMU WANAHARIBU MAZINGIRA
LAKINI WANATAKIWA KUJUA NA WAO HAWATAKUWA SALAMA!
Mchoraji: Musa Ngarango Jr.
150


HONGERA MWENZANGU, SIJUI MAJI UMEYAPATA WAPI
WE ACHA TU, NI MBALI SANA, TULINDE VYANZO VYA MAJI JAMANI UKAME UTATUMALIZA
Mchoraji: Musa Ngarango Jr.
152


KUTUPA TAKA HOVYO NAMNA HII KWENYE CHANZO CHA MAJI NI KITU KISICHOKUBALIKA
NI KWELI, JAMII KWA KUSHIRIKIANA PAMOJA TUNAPASWA KULINDA VYANZO VYETU VYA MAJI ILI VISICHAFULIWE NAMNA HII


MWANZO NILIKUWA SIJUI KAMA TAKA ZINAWEZA KUREJELEZEKA NA HATA WATU KUNUFAIKA KIUCHUMI KWA KUZIUZA
NI KWELI, MFANO TAKA ZA KIELEKTRONIKI MIMI NIMEPELEKA KWA MREJELEZAJI NA NIMEPATA FEDHA, HIVYO TUSITUPE TAKA HOVYO


JAMANI KWELI MITI NI UHAI, LAZIMA NA SISI TUUNGE MKONO ZOEZI LA UPANDAJI MITI
HATA NYUMBANI KWETU INABIDI TUKAPANDE MITI
TUPANDE MITI KWA WINGI, TUKIPANDA MITI NA KUTUNZA MAZINGIRA TUNAOKOA MAISHA YETU SISI WENYEWE
MCHORAJI:
Musa Ngarango Jr.
159


HATA SISI TUNAJALI NA KUTUNZA MAZINGIRA YETU, TUNAIASA JAMII TUSIKATE MITI HOVYO
NI KWELI, PIA TUSIINGIZE MIFUGO KWENYE VYANZO VYA MAJI
Mchoraji: Musa Ngarango Jr.
149




*Wasiliana nasi;*

**Mkurugenzi Mkuu,**

**Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC),**

Ghorofa ya 6, Jengo la Kambarage, Brabara ya PSPF S.L.P 2724, Dodoma, Tanzania.

Simu: +255 26 296 0098, +255 713 608 930

Barua pepe: dg@nemc.or.tz, Tovuti: www. nemc.or.tz


#MazingiraYetuUhaiWetu


Namba ya Bure: **0800110116**

@nemctanzania

NemcTVTanzania

www.nemc.or.tz